

# MWONGOZO WA MAZUNGUMZO KUHUSU CHANJO ZA COVID-19

Ngoja tuzungumze kuhusu chanjo za COVID-19





01

Utangulizi

# Kuhusu mwongozo huu

Mwongozo huu wa vitendo wa Mazungumzo utasaidia watoa huduma za makazi kuwa na mazungumzo kuhusu chanjo za COVID-19 na kujibu wasiwaso wa wateja kuhusu chanjo ya COVID-19 kuitia mbinu ya heshima na uthibitisho.

Mwongozo huu unasaidia watoa huduma za makazi kuwa na mazungumzo yanayofaa kuhusu chanjo ya COVID-19 kwa kuwasiliana na wateja na kusuluhisha masuala ambayo yanaweza kutokea wakati wa mazungumzo.

# Kuhusu mwongozo huu



Mwongozo huu unazingatia kuwa na mazungumzo kwa njia nzuri ya kujali ili kusikiliza na kuelewa sababu za kutopata chanjo, kujadili wasiwasi na kutatua maswali ili wateja waweze kuzingatia na kuelewa chanjo za COVID-19.

Mwongozo ulitengenezwa na Migration Council Australia (MCA) kwa ushirikiano wa karibu na SETSCoP — ushirikiano wa kitaifa wa watoa huduma wa makazi 112 ambao husaidia wahamiaji na wakimbizi chini ya mpango wa Settlement Engagement and Transition Support (SETS). SETSCoP inawezeshwa na MCA na inalenga katika kusaidia watoa huduma wa SETS kufanya kazi kwa ushirikiano katika kushughulikia masuala yaliyotambuliwa.

# Jitayarische kwa mazungumzo



Watoa makazi mara nyingi ndio watu wa mawasiliano wa kimsingi wa kupata huduma na habari. Hali hii haina tofauti katika mambo ya chanjo ya COVID-19.

Kuwa na mazungumzo kuhusu chanjo za COVID-19 kunaweza kusaidia kuweka jamii salama na kuchangia katika kupunguza madhara yanayohusiana na COVID-19 na kukomesha maambukizi ya ugonjwa huo.

Kushughulikia maswala kuhusu chanjo za COVID-19 inaweza kuwa mada yenye changamoto kwa kuwa baadhi ya masuala yanahusu uzoefu wa kibinafsi, imani, habari potofu na uzoefu wa zamani wa matibabu duni au yasiyo mazuri kwa afya.

# Jitayarische kwa mazungumzo



Kabla ya kuanza mazungumzo kuhusu chanjo za COVID-19 kuna baadhi ya mambo ambayo unaweza kufanya:

- Chagua wakati unaofaa kwako na mtu unayetaka kuzungumza naye. Ni muhimu kuchagua wakati na mahali ambapo nyote wawili mko vizuri.
- Weka njia nzuri na ya kirafiki.
- Kumbuka kwamba maoni yetu yanajengwa kulingana na mambo au hali tofauti.

Ikiwa wateja hawajisikii tayari kuzungumza, wajulishe kuwa utakuwa tayari kuzungumza nao ikiwa watahitaji usaidizi katika siku zijazo.



02

Kuwa na mazungumzo



## **1. Kuwa na huruma na ungana na maadili ya watu binafsi**

Dumisha ukarimu katika mazungumzo yote na ukubali maadili na hisia za mteja. Sio lazima ukubaliane na kila kitu, lakini unaweza kusaidia wengine kwa kuungana nao bila hukumu.



Nina wasiwasi kuhusu chanjo. Sijui  
taarifa za kutosha kuhusu hizo.

Ninalewa ni wakati mgumu, na ni sawa  
kuwa na maswali pamoja na kuhisi wasiwasi.



Ni nini kingekusaidia kujisikia vyema kuhusu chanjo ya COVID-19?

Nadhanu kuwa na habari zaidi kungenisaidia.



## 2. Uliza maswali ya wazi kuhusu wasiwasi wao

Uliza maswali ya wazi ambayo husaidia kutambua chanzo cha wasiwasi. Maswali haya yanaweza kukusaidia kuelewa wasiwasi za mtu mwingine vyema na yanaweza kumsaidia mtu huyo kutambua na kufafanua mawazo yake.

Hii pia ni njia nzuri ya kuelewa ni wapi walipata taarifa zao na jinsi walivyopata majibu ya maswali yao.



Sijisikii kujiamini kuhusu kupata chanjo  
ya COVID-19.

Ni nini kingekufanya uwe na uhakika zaidi  
kuhusu chanjo?

Ningependa kujua jinsi chanjo zinavyofanya kazi na kama zinaweza kubadilisha Asilia (DNA) yako.

Chanjo hufunza mfumo wako wa kinga kutambua na kupambana na virusi kama vile COVID-19. Chanjo za COVID-19 hutumia miiba ya virusi vya korona kusaidia mwili wako kutoa kingamwili zinazoweza kupigana na virusi. Haviwezi kubadilisha Asili (DNA) yako kwa njia yoyote.






### 3. Kuwa na mazungumzo ya kibinafsi na ya familia

Uamuzi wa chanjo unaweza kuwa chaguo la kaya ambapo mtoa maamuzi wa familia anachagua kwa ajili ya kaya, au inaweza kuwa uamuzi wa mtu binafsi. Unaweza kufanya mazungumzo na mteja binafsi au wanakaya wanaostahiki ili kujadili wasiwasi wao na motisha ya kupata chanjo.



Instructions:

- The words that we need to keep in English highlighted in **yellow**.
- The words in **green highlight**, should be translated and include the English words in brackets.



Baba yangu ndiye anaamua katika nyumba. Bado anachanganyikiwa kuhusu chanjo.

Ninaelewa. Vipi tujadili masuala haya pamoja?

- Instructions:
- The words that we need to keep in English highlighted in yellow.
  - The words in green highlight, should be translated and include the English words in brackets.

## 4. Shiriki habari inayoaminika


Shiriki kila wakati habari kutoka kwa vyanzo vya kuaminika.

Pindi tu unapokuwa na uhakika kuwa umeelewa maswali au mahangaiko yao, unaweza kuwaliza kama unaweza kushiriki nao taarifa zinazoaminika au kuwasaidia kutafuta taarifa au kuwasiliana na General Practitioner ( Daktari wa Familia) (GP).



Chanjo za COVID-19 zilitengenezwa kwa muda mfupi. Nitajuaje kuwa ziko salama?

Chanjo ya COVID-19 imefuata itifaki sawa na chanjo zingine. Wanasyansi kote ulimwenguni walifanya kazi pamoja kutengeneza chanjo za COVID-19 na kazi hii ya pamoja imewasaidia kuharakisha mchakato huo.





Ukipenda, ninaweza kushiriki nawe baadhi ya nyenzo, au tunaweza kutafuta maelezo zaidi.

Ndiyo, nadhani hiyo inaweza kuwa na manufaa.

## 5. Kuwasaidia wateja kupata sababu yao kupata chanjo


Kupata chanjo ni chaguo la kibinafsi na sote tuna sababu tofauti za kupata chanjo ya COVID-19. Hadithi yako ya kibinafsi inaweza kuwasaidia kupata sababu ya kupewa chanjo. Unaweza kushiriki sababu zako za kupata chanjo, ikiwa ulikuwa na wasiwasi wowote na jinsi ulivyohakikishiwa kuhusu chanjo.

Baadhi ya sababu za kupata chanjo ni, kwa mfano, kwamba tutaweza kuwatembelea wapendwa wetu ng'ambo na kutangamana bila woga wa kuugua sana iwapo tutashika virusi.



Kwa nini tupate chanjo ikiwa watu bado  
wanaweza kupata COVID-19 wakiwa  
wamechanjwa?

Ni kweli kwamba bado tunaweza kupata COVID-19 baada ya kupata  
chanjo. Lakini chanjo hizo ni nzuri sana katika kutulinda tusiwe  
wagonjwa sana na kulazimika kwenda hospitali au hata kufa.






Nilipata chanjo kwa sababu nilitaka kuwatembelea jamaa zangu salama katika majimbo mengine tena. Je unafikiria nini?



## **6. Kusaidia wateja kupanga miadi**



Ikiwa wataonyesha nia ya kuchanjwa, unaweza kuwasaidia wateja katika mchakato wa kusajili au kuweka miadi ya kupata chanjo. Unaweza kutumia Vaccine Clinic Finder ili kupata kliniki inayowafaa.

Ningependa kuweka miadi na kupata chanjo, lakini  
sina kadi ya Medicare.

Chanjo za COVID-19 ni bure kwa kila mtu nchini Australia. Huhitaji  
Medicare au hali fulani ya visa.



Je, ninaweza kwenda wapi kupata chanjo?

Nikusaidie kupata mahali pazuri pa kupata chanjo.



03

Ni wapi pa kupata habari

# Department of Health

Tovuti ya Department of Health inatoa anuwai ya nyenzo zilizotafsiriwa katika lugha 63 za jamii. Tovuti hii hutoa maelezo kuhusu chanjo ya COVID-19 kama vile jinsi ya kupata chanjo, madhara, habari potofu na maswali yanayoulizwa sana. Unaweza pia kupata video, jumbe za redio, karatasi za ukweli, mabango na rasilimali za mitandao ya kijamii.

Unaeweza kupata habari zaidi hapa

<https://www.health.gov.au/initiatives-and-programs/covid-19-vaccines/covid-19-vaccine-information-in-your-language>


# COVID-19 Vaccine Clinic Finder



The [COVID-19 Vaccine Clinic Finder](#) ni zana ya mtandaoni ambayo hutoa taarifa katika lugha 15 za jumuiya kuhusu wakati na mahali unapoweza kupokea chanjo ya COVID-19 na hukuruhusu kuweka miadi katika kliniki ya chanjo iliyo karibu nawe.

Unaweza kupata habari zaidi hapa  
[health.gov.au/covid19-vaccines-languages](https://health.gov.au/covid19-vaccines-languages)

# National Coronavirus Helpline



[National Coronavirus Helpline](#) hutoa maelezo kuhusu chanjo ya COVID-19 na inaweza kukusaidia kupata kliniki ya chanjo na kutoa maelezo ya mawasiliano ili uweke nafasi.

Unaweza kupigia simu National Coronavirus Helpline kwa 1800 020 080. Huduma hii inapatikana kwa masaa 24 siku 7 kwa wiki.

Kwa huduma za ukalimani pigia simu TIS National on 131 450 na uliza kuunganishwa na National Coronavirus Helpline.

# **Idara za Afya za Mikoa/Majimbo**




Mikoa na majimbo pia yametengeneza rasilimali zilizotafsiriwa zenye maelezo kuhusu chanjo ya COVID-19.


- [ACT](#)
- [NSW](#)
- [QLD](#)
- [SA](#)
- [TAS](#)
- [VIC](#)
- [WA](#)
- [NT](#)

# RANZCOG

The Royal Australian and New Zealand College of Obstetricians and Gynaecologists (RANZCOG) hutoa taarifa za sasa na mwongozo kuhusu chanjo za COVID-19 kwa wanawake wajawazito au wanaonyonyesha na wale wanaopanga kupata mimba kulingana na ushauri wa Australian Technical Advisory Group on Immunisation (ATAGI).



# Healthdirect



Healthdirect hutoa taarifa za afya na ushauri kuhusu chanjo za COVID-19 vaccine. Tovuti yake inatoa taarifa kwa Kiingereza kwa ajili ya maswali yanayoulizwa mara kwa mara. Hii inajumuisha COVID-19 Vaccine Side Effects Symptom Checker ambayo yanasaidia kwa wasiwasi mbalimbali ambazo zinahusiana na madhara ya kupata chanjo za COVID-19.

Unaweza kupata habari zaidi

<https://www.healthdirect.gov.au/coronavirus>

# MyAus COVID-19 App

The [MyAus COVID-19 App](#) ni programu ya bure iliyotengenezwa na Migration Council Australia ambayo inatoa habari na usaidizi wa COVID-19 katika lugha 29 za jumuiya, ikijumuisha maelezo kuhusu chanjo ya COVID-19 katika lugha inayoweza kufikiwa

